

MTIHANI WA MWIGO WA PTE 2019

KISWAHILI 1013/2

MUDA: SAA 2

FASIHI NA MBINU ZA KUFUNDISHIA

MAAGIZO

- i. Mtihani huu una sehemu **mbili** kuu: sehemu ya **A – FASIHI** and sehemu ya **B - MBINU ZA KUFUNDISHIA**.
- ii. Jibu maswali matatu katika sehemu ya A. Swali la kwanza ni la lazima. Chagua maswali mengine mawili kutoka kwa swali la 2, 3, au la 4. (Tamthilia, Riwaya au Hadithi Fupi).
- iii. Usijibu maswali mawili kutoka kwa kitabu kimoja.
- iv. Jibu maswali yote kutoka sehemu ya B.
- v. Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwazoni mwa kila sehemu.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

| SEHEMU | SWALI | UPEO | ALAMA |
|---------------|--------------|-------------|--------------|
| A | 1 | 15 | |
| | 2a | 15 | |
| | 2b | 15 | |
| | 3a | 15 | |
| | 3b | 15 | |
| | 4a | 15 | |
| | 4b | 15 | |
| B | 5 | 15 | |
| | 6 | 20 | |
| | 7 | 20 | |
| | JUMLA | 100 | |

MANENO MUSIRUKIE

Kurukia si kuzuri, maneno musirukie,
Mutakuja zusha shari, makonde muyabugie,
Mukimbie kwa ghururi, kama kuku mukimbie,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.

Wasemapo majabari, meneno musirukie,
Hasa walio jeuri, kamwe musikukurubie,
Ndondi zitawaaziri, na kwa Mola mutubie,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.

Hii nayo ni kiburi, litemwalo murukie,
Yafaa mujihadhari, gumzo mulisike,
Musije watu hasiri, magumi yawashukie,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.

Imezukapo hatari, hii leo nikwambie,
Msemaji mhadari, uhodari ajitie,
Kapambana na jabari, la kufanya asijue,
Maneno musirukie, wasemapo majabari.

Kabla ujafikiri, jitu limgeukie,
Likamzaba hodari, naye mbio akimbie,
Likamkazia shari, na mbio asizijue,
Maneno mushirukie, wasemapo majabari.

SEHEMU A – FASIHI

Ushairi

Hili ni shairi la ina gani? Toa sababu yako. (alama 2)

Eleza umbo la shairi hili. (alama 2)

Eleza maudhui ya shairi hili. (alama 6)

Ziandike beti mbili za mwisho katika lugha ya nadhiri. (alama 4)

Taja bahari ya shairi hili. (alama 1)

Tamthilia

Upeo wa mvua na Jeff Mandila

“.....tunanga’ngania mlo kama mapaka na majibwa. Sasa ni jioni kuanzia alfajiri,
hatujala chochote na mzigo huu wote.....”

(a)(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Eleza sifa zozote **saba** za mnenewa (alama 7)

(iii) Kwa kutoa hoja **nne** mwafaka eleza vile mtunzi amefaulu kutumia mbinu ya sadfa kufanikisha kazi yake. (alama 4)

(b) Fafanua umuhimu wa kidani katika kuendeleza tamthilia ya upepo wa mvua. (alama 15)

PENDO LA KARAHA - RIWAYA

3. (a) Pendo la Karaha ni Riwaya inayoangazia changamoto zinazokabili umma. Jadili. (alama 15)

Au

Riwaya ya Pendo la Karaha imeshughulikia maudhui ya mabadiliko. Thibitisha.

(alama 15)

4. (a) Na Pauline Kea Kyovi (Kenya) – VAZI LA MHUDUMU

Eleza maudhui makuu **manne** yaliyojadiliwa katika hadithi. (alama 8)

(b) Huku ukirejelea hali halisi, onyesha njia mbadala ambayo wahudumu wa kidini wanavyodhihirisha unafiki. (alama 1)

(c) Jadili upotevu wa maadili unaodhihirika katika jamii iliyotungiwa hadithi hii. Jadili tatu. (alama 6)

5. (a) Mwalimu mwenza ana mtazamo hasi kutumia vifaa kufanikisha somo. Umshawishi na hoja **tano** abadili mtazamo huu. (alama 5)

(b) Pendekeza vifaa **vitano** mwafaka mwalimu atatumia kufanikisha somo la sarufi ngeli ya YA-YA. (alama 5)

(c) Taja udhaifu wa chati kama kifaa cha kufunzia. (alama 5)

KUZILIZA NA KUZUNGUMZA

6. (a) Eleza umuhimu wa kufunza kwa mwanafunzi wa darasa la pili. (alama 10)

(b) Fafanua jinsi mwanafunzi anavyoweza kukabiliana na ukosefu wa vitabu nyanjani. (alama 10)

7. Kwa kurejelea andao la somo la Kiswahili, andaa vile utakavyofunza kipindi cha kusoma herufi kwa mwanafunzi wa darasa la kwanza. (alama 20)
